**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MATOMBO 2023

**Juni, 2023**

**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Namba za Simu 0762412377**

**Mkuu wa Shule 0714907572**

**Makamu Mkuu wa Shule 0716600067**

**Matron/Patron 0714806267**

**Shule ya Sekondari Matombo**

**S.L.P 749 Morogoro**

**Tarehe 12/06/2023**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MATOMBO HALMASHAURI YA WILAYA MOROGORO MKOA WA MOROGORO MWAKA 2023/24**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2023 na atasoma tahasusi ya HGL au HKL(Kata isiyohusika)

Shule ya Sekondari Matombo ipo umbali wa Kilometa 64 Kusini mwa Mji wa Morogoro Usafiri wa basi kutoka mjini Morogoro unapatikana katika kituo cha mabasi Msamvu au Karoleni Nauli ni Shilingi 7,000/= kwa gari.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 14/08/2023, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 13/08/2023 Mwisho wa kuripoti ni tarehe 31/08/2023.

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

i. Sare ya shule hii ni sketi ya dark bluu mbili (02) za rinda box kwa Wasichana na (zinapatikana Jirani na shuleni kwa Tsh 25,000/= kwa pea moja)
ii. Mashati mawili meupe ya mikono mifupi (yanapatikana Jirani na shule kwa gharama ya Tsh 12,000 kwa shati moja).
iii. Rangi ya Hijab (kijuba) ni nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama. Pia kwa ajili ya kuleta ulinganifu wa kitambaa na mshono sawia kwa wanafunzi wote wa kike (Yanapatikana jirani na shuleni kwa gharama ya Tsh 15,000/- kwa pea moja)
iv. Sare ya Michezo ni track suit pea moja ya dark bluu (inaweza kupatikana Jirani na shuleni kwa gharama ya Tsh 30,000/=)
v. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
vi. Soksi jozi mbili nyeupe;
vii. Sweta la dark bluu
viii. Nguo za kushindia ni sketi mbili za visanduku ya rinda box ( unaweza kuipata Jirani na shuleni kwa gharama ya TSH 20,000/=
ix. Tisheti moja au mbili za form six za rangi ya bluu ( inapatikana Jirani na shuleni kwa gharama ya Tsh 12,000/ kwa kila moja).

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari ya kaunta book tisa

ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka na rulled paper ( karatasi za mistari mbili (02) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha iambatishwe*);
iv. Scientific Calculator;
v. Godoro lenye vipimo vya 2.5x6
vi. Mashuka ya rangi ya pinki Jozi 2, blanket 1, mto na foronya ya mto 1, chandarua 1 cheupe;
vii. Nguo za ndani za kutosha;
viii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
ix. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
x. Kwanja 1, jembe 1, reki 1, sabuni ya maji lita moja na mifagio 2 wa ndani na nje.

### 2.3 Michango mbalimbali

**a) Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Malipo yafanyike kupitia akaunti namba 22101100129 jina Matombo Secondary School Benki ya NMB**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- ❖ **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- ❖ **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;

iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule**

**Jina la Mkuu wa Shule MARIAM R MADAMBA**
**Mhuri wa Mkuu wa Shule**

THE HEADMISTRESS
MATOMBO SEC. SCHOOL
P. O. BOx 749
MOROGORO

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0714 907 572**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0716 600 067**
- **Mwandamizi Taaluma 0655 182 992**
- **Mwandamizi Malezi 0762412377**

## Kiambatanisho vya mshono wa sketi na Tshirt



Kiambatanisho  cha rangi na muonekano wa Sare za michezo zikiwa na nembo na utambulisho maalumu.



**AHADI YA MWANAFUNZI**

Mimi……………………………………………………………………………………………………………………

Nimesoma na kuelewa yote yaliyoelekezwa kwenye barua ya kujiunga na shule.

Ninaahidi kuwa nitajifunza kwa bidii zangu zote, nitazingatia sheria za shule kama zilivyoainishwa, nitazifuata na nitakuwa na nidhamu wakati wote kwa manufaa yangu, ya shule na ya taifa kwa jumla.

| | | |
|---|---|---|
| ……………………………… | …………………….. | ………………………………… |
| **Saini ya Mzazi/Mlezi** | **Tarehe** | **Saini ya Mwanafunzi** |

## FOMU YA HISTORIA YA MWANAFUNZI

1. JINA LA MWANAFUNZI.................................................................................................

2. JINA LA MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI..............................................................

3. JINA LA SHULE ANAKOTOKA......................................................................................

4. TAREHE YA KUZALIWA...............................................................................................

5. KATA ANAYOTOKA MWANAFUNZI...........................................................................

6. WILAYA ANAYOTOKA MWANAFUNZI......................................................................

7. MKOA ANAOTOKA MWANAFUNZI...........................................................................

8. KABILA.........................................................................................................................

9. URAIA...........................................................................................................................

10. DINI/DHEHEBU............................................................................................................

11. ANUANI YA MZAZI/MLEZI..........................................................................................

12. NAMBA YA SIMU YA MZAZI/MLEZI - NYUMBANI...................................................
- OFISINI.......................................................
E - MAIL ADRESS...............................................................................................
ANUANI YA POSTA KWA AJILI YA KUTUMA MATOKEO YA MITIHANI: -
....................................................................................................
....................................................................................................

8

13. MAJINA MANNE YA NDUGU WA KARIBU WALIOIDHINISHWA KUCHUKUA NAFASI YA MZAZI/MLEZI ENDAPO DHARURA ITATOKEA:-

| **Na** | **JINA** | **UHUSIANO** | **ANAKOISHI** | **NAMBA YA SIMU** |
|---|---|---|---|---|
| 01. | | | | |
| 02. | | | | |
| 03. | | | | |
| 04. | | | | |

Secondary School Education.

a). Eye sight ..........................................
b). Hearing ..........................................
c). Limbs ..........................................
d). Speech ..........................................
e). Venereal diseases ..........................
f). Leprosy..........................................
g). Epilepsy..........................................
h). Neurosis..........................................
i). Other serious diseases........................
j). Pregnancy..........................................

Name........................................................ Signature.......................... Date..........................